JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MWONGOZO WA UPIMAJI WA MWAKA

policy forum

MFUMO WA RUZUKU YA MAENDELEO

YA SERIKALI ZA MITAA (LGDG)

Vifupisho

CBG	Ruzuku ya Kujenga Uwezo
CDG	Ruzuku ya Maendeleo ya Halmashauri
CMT	Menejimenti ya Halmashauri
KM-OR-TAMISEMI	Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
LGDG	Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa
MCs	Vigezo vya Msingi
MEG	Ruzuku ya Ufuatiliaji na Tathmini
MSM	Mamlaka ya Serikali za Mitaa
OR-TAMISEMI	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
PMs	Vigezo vya Kiutendaji
ToRs	Hadidu za Rejea

Upimaji wa Mwaka

Utangulizi

Upimaji wa Mwaka wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni zoezi lililoanzishwa na Mfumo wa Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG) kupima utendaji kazi wa kila Halmashauri kwa kila mwaka ili kuamua kiasi cha fedha cha LGDG ambacho hatimaye kitapelekwa kwenye Halmashauri husika kwa kuzingatia matokeo ya upimaji huo.

Malengo ya Upimaji:

a) kuhakikisha kuwa fedha za LGDG zinatumika vizuri, kwa mujibu wa sheria na taratibu za Serikali ya Tanzania.
b) Kujua viwango vya utendaji wa Serikali za Mitaa katika kuboresha utoaji wa huduma.
c) kuzipa motisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazo fanya vizuri ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi wao kwa mujibu wa mfumo wa tuzo na adhabu.

Vigezo vya Upimaji

Kuna vigezo viwili vya Upimaji ambavyo ni:

1. **Vigezo vya Msingi (MCs**); Ni vigezo ambavyo viliwekwa ili kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatumia vizuri fedha wanazoletewa kwa ajili ya miradi yao ya maendeleo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali kama vile Sheria ya Serikali za Mitaa sura ya 287 na 288, Sheria za fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290, Kanuni ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009, Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011(iliyofanyiwa marekebisho 2016).

2. **Vigezo vya Kiutendaji (PMs**); Ni vigezo vinavyolenga kuhamasisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa kufanya vizuri katika utoaji wa huduma bora. Serikali za Mitaa ambazo zinafanya jitihada kubwa zaidi ya kuzitumikia jamii zake kwa ufanisi zitapewa tuzo wakati Serikali za Mitaa zenye utendaji wa kiwango cha chini zitazuiliwa fedha zao mpaka zitakapo boresha hali hiyo. Kushindwa kuboresha kasoro zilizo jitokeza kutapelekea kuchukuliwa hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi walio husika.



ZINGATIA: - Tofauti na Vigezo vya Msingi (MCs); Vigezo vya Utendaji (PMs) vinalenga zaidi kwenye matokeo na vinalenga kutathmini utendaji wa Serikali za Mitaa katika maeneo tisa kati ya 10 ya Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa ya mfumo wa LGDG kama ilivyoelezwa kwenye *Mwongozo wa Utekelezaji na Uendeshaji.* Matokeo namba saba (7), ambayo yanasema kwamba 'Fedha za Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa zitengwe na kugawiwa kwa usahihi kwenye Serikali za Mitaa, ' halijumuishwi kwa kuwa linahusiana na Serikali Kuu, hivyo siyo lengo mahususi kwenye tathmini ya utendaji wa Serikali za Mitaa.

Zoezi la Upimaji

Zoezi hili litafanywa kwenye kila Halmashauri kati ya mwezi Agosti na Septemba na matokeo ya upimaji (ikiwa ni pamoja na mgao wa ruzuku) yatatolewa kwa kila Halmashauri mwezi Novemba mwaka huo huo. Hii itaziwezesha Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuandaa mipango yao na bajeti ya kila mwaka kwa kuzingatia matokeo ya upimaji.

Timu ya upimaji ya mkoa itaundwa na kikosi kazi cha Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa. Timu hiyo ya upimaji ya mkoa itakuwa timu ya upimaji ya Halmashauri katika mfumo huu. Itakuwa inajumuisha maafisa kutoka Sekretarieti ya Mkoa (ingawa siyo kutoka katika mkoa huo huo ambao Halmashauri zitapimwa) pamoja na baadhi kutoka kwenye taasisi nyingine za umma. Timu ya upimaji itajumuisha maafisa watatu kutoka sekretarieti ya mkoa na wawili kutoka katika taasisi za umma ndani ya mkoa.

Upimaji utaanza na vigezo vya msingi vilivyokubaliwa vilivyopo kwenye Ruzuku ya Maendeleo ya Halmashauri (CDG). Baada ya hapo, upimaji utafanywa kwenye vigezo vya kiutendaji (PMs) kwa kila kiashiria katika maeneo yote tisa (9) ya matokeo kwa kutumia kipimo cha alama. Ruzuku ya Kujenga Uwezo (CBG), kwa kiasi kikubwa, inatarajiwa kushughulikia mapungufu ya utendaji yaliyobainishwa kwenye tathmini ya utendaji. Kutokana na matokeo ya upimaji, marekebisho kwenye mgao wa fedha za LGDG kwa kila Halmashauri yatafanywa.

Mabadiliko Makuu Katika Upimaji wa Mwaka

Mabadiliko Makuu Yaliyofanywa Kwenye Mapitio ya Sasa Kwenye Suala la Upimaji wa Mwaka

Baadhi ya mabadiliko yamefanywa kwenye mchakato wa upimaji wa mwaka kwenye mapitio haya kutokana na changamoto zilizoonekana wakati wa utekelezaji wa mfumo huu miaka iliyopita. Maboresho haya yamezingatia hasa hitaji la kuwepo ufuatiliaji wa karibu sana unaofanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na tathmini makini zaidi ili kuwaongoza kwenye utekelezaji. Pia, upimaji utaongoza na kuonesha aina ya utendaji ambao Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinapaswa kuwa nao, pamoja na kuhimiza kujengeana uwezo wa ndani ili kuwe na uendelevu badala ya kutegemea wataalamu-washauri kutoka nje ya halmashauri kama ilivyokuwa ikifanyika.



Uhusiano na Zoezi la Ufuatiliaji Unaofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya upimaji wa mwaka na ufuatiliaji wa maendeleo ya utekelezaji wa shughuli za LGDG zinazofanywa mara kwa mara na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Uhusiano huu upo kwa maana kwamba, ufuatiliaji utakaofanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa unashughulikia karibu nyanja zilezile au maeneo yote muhimu yatakayo pimwa wakati wa tathmini ya mwaka. Hivyo, Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambazo zinafanya jitihada sahihi za kufanya ufuatiliaji makini wa mipango yao ya LGDG na miradi zitakuwa na nafasi nzuri ya kupata alama za juu kwenye upimaji wa mwaka.

Mchakato wa Upimaji wa Mwaka wa Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa

Upimaji wa Mwaka

Upimaji wa kila mwaka wa utendaji wa kila Halmashauri utafanywa chini ya mwamvuli wa OR-TAMISEMI kupitia Timu za Upimaji za Mikoa. Matokeo ya upimaji yatabaini Halmashauri ambazo zinahitaji kusaidiwa ili ziweze kutoa huduma bora.

Kielelezo cha Mchakato wa Upimaji



Wajibu wa kufanya Upimaji wa Mwaka kwenye Halmashauri

OR-TAMISEMI itawajibika kikamilifu kuandaa na kuratibu upimaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Itawajibika kuhakikisha kuwa zoezi la upimaji la LGDG linakuwa wazi lenye malengo na mchakato huru wa upimaji kwa kufanya yafuatayo: kuunda Kamati ya Ufundi ya Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG) kwa kushirikiana na Kamati Tendaji ya Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa ya Taifa, kuunda Kikosi Kazi cha upimaji wa Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa na kuandaa Hadidu za Rejea (TORs) za kikosi kazi na programu elekezi kwa wajumbe wake.

Mwongozo wa Hatua za Upimaji wa Mwaka

Mhusika	Shughuli/Kazi	Muda	Maelezo
Maandalizi na Upimaji			
OR- TAMISEMI (Sekretarieti ya LGDG).	• Kutenga bajeti kwa ajili ya zoezi la upimaji wa MSM kupitia MEG.	Julai – Juni ya mwaka wa fedha uliopita.	
	• Kuunda, kutoa maelekezo na kuandaa ToR kwa kikosi kazi cha Upimaji cha LGDG. • Kuandaa programu elekezi kwa ajili ya Timu za Upimaji. • Kuamua kuhusu mpangilio wa zoezi la upimaji. • Kuzifahamisha sekretarieti za mikoa kuhusu ratiba ya zoezi la upimaji na uteuzi wa wajumbe wa Timu za Upimaji za Mikoa. • Kuthibitisha wajumbe wa Timu za Upimaji.	Julai.	Mwongozo wa Upimaji wa LGDG.
Kikosi kazi cha Upimaji wa LGDG.	• Kuratibu zoezi la Upimaji. • Kutoa mafunzo elekezi kwa Timu za Upimaji. • Kutoa mpangilio wa maeneo ya kwenda kufanyia kazi na taratibu za kiutawala.	Julai – Agosti.	Mwongozo wa Upimaji wa LGDG.
Timu za Upimaji za Mikoa.	• Kuhudhuria mafunzo/semina elekezi. • Kujipanga kwa ajili ya zoezi la upimaji na zana zitakazotumika.	Agosti.	Mwongozo wa Upimaji wa LGDG.
Ngazi za juu na ngazi za msingi.	• Kuandaa nyaraka na taarifa zote zinazotakiwa kwa ajili ya timu za tathmini na kuzifahamisha ngazi za msingi kufanya vivyo hivyo.	Agosti.	Mwongozo wa Upimaji wa LGDG.
Upimaji wa Utendaji Kazi wa MSM Dhidi ya Vigezo vya Msingi (MCs) na vya Kiutendaji (PMs) na Utekelezaji wa Mpango wa Kujenga Uwezo			
Timu za Upimaji za Mikoa.	• Kufanya Upimaji katika kila MSM ngazi za juu na za msingi kama ilivyoelekezwa kwenye mwongozo, yaani kuzifikia MSM kuona utekelezaji wa vigezo vya msingi na vya kiutendaji na utekelezaji wa mpango wa kujenga uwezo. • Kufanya vikao vya utangulizi na kutoa mrejesho kwenye timu ya menejimenti ya Halmashauri.	Agosti.	Mwongozo wa Upimaji wa LGDG.
Maandalizi ya Taarifa			
Timu za Upimaji za Mikoa.	• Kuandaa taarifa za kila MSM na kuwasilisha kwenye kikosi cha LGDG cha upimaji. • Kuandaa taarifa ya ujumla ya upimaji kwenye Mkoa (Kiongozi wa Timu).	Agosti.	Mwongozo wa Upimaji wa LGDG.

Mhusika	Shughuli/Kazi	Muda	Maelezo
Maandalizi na Upimaji			
MSM.	• Kufanya majadiliano kwa minajili ya kupokea taarifa ya upimaji na kupanga mikakati ya kukabiliana na mapungufu.	Agosti.	Mwongozo wa Upimaji wa LGDG.
Maandalizi ya Taarifa			
Maandalizi ya Taarifa na Uidhinishaji			
OR- TAMISEMI, Sekretarieti ya LGDG, kikosi kazi cha Upimaji.	• Kupitia taarifa za kila MSM. • Kufanya ufuatiliaji na uhakiki kwa kushirikiana na Timu ya Upimaji ya Mkoa (kiongozi wa Timu) kwa ajili ya kupata ufafanuzi wa masuala yatayojitokeza. • Kuandaa taarifa ya kitaifa.	Septemba.	Mwongozo wa Upimaji wa LGDG.
	• Kuwasilisha taarifa iliyohakikiwa ya kila MSM na taarifa ya kitaifa kwenye kamati ya kitaalamu.	Septemba.	
Kamati ya kitaalamu.	• Kuchambua taarifa za Upimaji kubaini MSM zilizokidhi MCs na PMs na kutoa ushauri kwenye kamati kuu ya kitaifa.	Oktoba.	
Kamati Kuu ya Kitaifa.	• Kuidhinisha taarifa za upimaji.	Oktoba.	
OR- TAMISEMI/ Sekretarieti ya LGDG.	• Kusambaza taarifa ya matokeo iliyoidhinishwa ya kila Halmashauri na taarifa ya kitaifa kwenye MSM na wadau wengine.	Oktoba.	
Maandalizi ya Bajeti ya LGDG na Utoaji wa Fedha			
OR- TAMISEMI.	• Kuandaa bajeti ya LGDG.	Novemba.	OR- TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango, Miongozo ya Mipango na Bajeti ya Hazina na OR-TAMISEMI.
	• Kuamua ugawaji wa Fedha kwa kuzingatia kanuni ya mgao iliyoridhiwa.	Novemba.	OR- TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango. Miongozo ya Mipango na Bajetiya Hazina na OR TAMISEMI.
Kamati ya Kitaalamu.	• Kupitia na kutoa mapendekezo kwa kamati kuu ya kitaifa.	Novemba.	
Kamati Kuu ya Kitaifa.	• Kufanya mapitio na kuidhinisha mgao wa ruzuku kwa MSM.	Novemba.	
Uhabarishaji na Usambazaji wa Taarifa			
OR – TAMISEMI.	• Kuchapisha muhtasari wa matokeo kwenye magazeti.	Novemba.	Mwongozo wa Upimaji wa LGDG.
MSM.	• Kupeleka taarifa ya kiasi cha mgao wa CDG, CBG na MEG kwenye ngazi za msingi.	Novemba.	


TAARIFA YA UPIMAJI IMETOKA HALMASHAURI YETU IMEFANYA VIZURI KATIKA MIRADI!
TAARIFA YA UPIMAJI
NGOJA NIKANUNUE GAZETI ILI NIISOME VIZURI NYUMBANI!
Regis

Vigezo vya Kugawa Ruzuku ya Maendeleo ya Halmashauri (CDG)

1. Ili Halmashauri iweze kupata asilimia 100 ya Ruzuku ya Maendeleo ya Halmashauri (CDG), ni lazima ifikie asilimia 80 ya vigezo vya msingi vilivyokubalika (MCs) na kupata alama zisizo pungua asilimia 50 katika kila kigezo cha utendaji (PMs).
2. Halmashauri 20 zinazofanya vizuri zaidi, yaani, zile ambazo zinafikia vigezo vya msingi (MCs) na kupata alama kuanzia asilimia 85 kwenye vigezo vya utendaji (PMs) zitapewa tuzo.
3. Halmashauri zinazokidhi vigezo vya msingi lakini zinashindwa kwenye vigezo vya kiutendaji; yaani, zimepata chini ya asilimia 50 ya eneo lolote la matokeo zitapokea asilimia 90 ya Ruzuku ya Maendeleo ya Halmashauri.
4. Halmashauri inayoshindwa kufikia asilimia 80 ya vigezo vya msingi lakini imepata asilimia 50 kwenye vigezo vya kiutendaji pia zitapokea asilimia 90 ya Ruzuku ya Maendeleo ya Halmashauri.
5. Halmashauri zilizoshindwa kwenye maeneo yote mawili ya vigezo vya msingi na vigezo vya utendaji zitapata asilimia 80 ya kiasi cha Ruzuku ya Maendeleo ya Halmashauri.

Vigezo vya Kugawa Ruzuku ya Kujenga Uwezo (CBG)

1. Halmashauri lazima zikidhi Masharti yote ya vigezo vya msingi ili kupata sifa za kupatiwa Fedha za Kujenga Uwezo.
2. Kama Halmashauri imeshindwa kukidhi vigezo vya msingi, itapokea asilimia 90 ya Ruzuku ya Kujenga Uwezo.
3. Kama sababu ni kutokana na uzembe, matumizi mabaya ya fedha n.k., maafisa husika watawajibishwa; na hatua stahiki za kinidhamu zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.
4. Vinginevyo, fedha zitazuiliwa mpaka hatua za kupata ufumbuzi wa tatizo zichukuliwe.

KUMBUKA: Kunavigezo Vitatu vya Msingi kwa Ruzuku ya Kujenga Uwezo:

1. Kuwa na Mpango wa kujenga Uwezo ulioboreshwa kutokana na Upimaji wa Mahitaji ya Kujenga Uwezo au Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ngazi ya juu (Halmashauri) na Serikali za Mitaa ngazi ya msingi (Kata, Mtaa/Kijiji na Kitongoji).
2. Kuwepo kwa ushahidi kwamba asilimia 60 ya Ruzuku ya Kujenga Uwezo zilitumika kwa ajili ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ngazi ya msingi.
3. Matumizi ya Ruzuku ya Kujenga Uwezo yalitumika kwa mujibu wa mwongozo wa Uwekezaji wa Ruzuku ya Kujenga Uwezo.

Mchakato wa Upimaji Utakaofanywa na Timu za Upimaji za Mikoa Katika kila Halmashauri ni kama Ifuatavyo:

Uundaji wa Timu za Upimaji za Mikoa.	• Inajumuisha watu watano (5), watatu (3) kutoka Sekretarieti ya Mkoa na wawili (2) ni wataalamu kutoka taasisi za umma wenye uzoefu/taaluma ya eneo husika. Mmoja wao atakuwa kiongozi wa timu ambaye atakuwa na uzoefu katika tawala za Serikali za Mitaa, mawasiliano na uandishi wa ripoti.
Mafunzo elekezi kwa Timu za Upimaji za Mikoa.	• TAMISEMI itatoa mafunzo elekezi kwa Timu za Upimaji za Mkoa kwa siku zisizozidi mbili (2). • Mafunzo elekezi yatahusisha vikao vya kuanza na kukamilisha zoezi, mbinu za upimaji katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ngazi ya juu na ngazi ya msingi.
Maandalizi kwa ajili ya kufanya kazi kwenye maeneo husika.	Yatafanyika kabla ya kuanza kazi kwenye maeneo husika kama ifuatavyo: • Kuandaa madodoso ya upimaji. • Kuandaa orodha ya miradi iliyotekelezwa. • Kuwasilisha ratiba iliyopendekezwa kwa ajili ya upimaji. • Kuandaa taarifa muhimu kwa mujibu wa dodoso la upimaji. • Kwenda kujitambulisha kwa viongozi waandamizi wa mkoa husika.
Kazi yenyewe kwenye maeneo husika.	• Kazi ya upimaji kwenye maeneo husika itachukua muda wa siku nne (4) kwa kila Halmashauri, ikigawanywa sawa kati ya Serikali za Mitaa ngazi ya juu na Serikali za Mitaa ngazi ya msingi. • Kwa kuanza na kikao cha utambulisho na Timu za Upimaji za Mikoa na Menejimenti ya Halmashauri (CMTs). • kupitia programu ya zoezi zima la upimaji. • kupitia nyaraka mbalimbali. • kufanya mahojiano na watoa taarifa muhimu kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ngazi ya juu na Serikali za Mitaa ngazi ya msingi. • kuthibitisha taarifa za Halmashauri zilizopokelewa kutoka Sekretarieti ya Mkoa. • Kukusanya taarifa na takwimu zinazohitajika ili kukamilisha mchakato wa upimaji. • Na kuandaa taarifa ya upimaji.

Mfumo wa kutoa Alama

Ili Halmashauri iweze kupata fedha za LGDG, ni lazima ikidhi vigezo vya msingi na vigezo vya utendaji. Kwahiyo, Timu za Upimaji za Mkoa zinatakiwa kupima endapo Halmashauri husika zina sifa stahiki kwa mujibu wa vigezo hivi.

Utoaji alama kwa vigezo vya msingi unategemea kigezo cha "Ndiyo" au "Hapana", yaani "Ndiyo" kama imekidhi vigezo au "Hapana" kama haijakidhi vigezo. Alama za "Ndiyo" au "Hapana" ni lazima ziwe na ushahidi na kuungwa mkono na taarifa na takwimu za kuaminika na za sasa. vigezo vya utendaji vinapimwa kwa kipimio kinachoanzia asilimia 0 hadi 100 (0-100%), asilimia 100 inaonesha kiwango cha juu kabisa cha utendaji bora unaoweza kufikiwa.

Ili Timu ya upimaji ifikie hitimisho la kutoa alama, ni lazima itafute taarifa zote muhimu kutoka Halmashauri, ifanye ukaguzi kwenye vituo vya huduma na kupata maoni ya watu inapobidi.

Upangaji wa Alama za Kipimo cha Utendaji kwa Kuangalia Maeneo ya Matokeo

Maeneo ya Matokeo	Jumla ya alama	Alama za chini zinazohitajika ili kupata fedha zote za Ruzuku ya Maendeleo ya Halmashauri (CDG)
1. Miradi inayofadhiliwa na LGDG inafanya kazi kwa ufanisi na kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi.	20	10
2. Vipaumbele vya jamii vinazingatiwa.	15	7.5
3. Jitihada za jamii zinatambuliwa, kuwezeshwa na kupewa usaidizi, kwa mtizamo wa kuunga mkono juhudi za Serikali kwa ajili ya utoaji wa huduma bora kwa wananchi.	8	4
4. Fedha zinatolewa kwa usawa ndani ya MSM.	10	5
5. Usimamizi wa fedha wa MSM unaboreshwa.	10	5
6. Maeneo yenye mazingira magumu yanafaidika kutokana na miradi yenye ubora inayotekelezwa na MSM.	10	5
7. Fedha za bakaa kwenye MSM zinatolewa taarifa na kufuatiliwa kwa karibu.	10	5
8. Rasilimali watu katika MSM inaendelezwa na kusimamiwa.	7	3.5
9. LGDG inasimamiwa kwa uwazi na uwajibikaji.	10	5
Jumla	**100**	**50**



Uchambuzi wa Takwimu na Utoaji wa Taarifa

Uchambuzi wa takwimu kuhusu vigezo vya msingi na vigezo vya utendaji na uunganishaji wa taarifa ya upimaji ya Mamlaka za Serikali ya Mitaa utafanyika wakati wa upimaji kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

(i) Takwimu na taarifa za kuhakiki kila kiasharia cha MCs na PMs zitapatikana kupitia nyaraka, ziara za kuona kwa macho maeneo ya kutolea huduma na mahojiano na watoa taarifa.



Wajumbe wa timu ya mkoa ya upimaji

(ii) Timu itaunganisha matokeo ya kila kiashiria kwa kila mwisho wa siku ya kazi kwa kufanya vikao na kujadili taarifa iliyopatikana.

(iii) Timu pia itajadili na kuweka kumbukumbu za masuala muhimu au yaliyoonekana ambayo yameathiri utekelezaji wa shughuli (mfano, mifarakano ya kisiasa na kijamii). Vivyo hivyo, matatizo yaliyopatikana wakati wa zoezi la upimaji (mfano, kutofika kwenye ngazi za msingi, kutopatikana kwa takwimu na taarifa, ushirikiano hafifu) lazima yatolewe taarifa.

(iv) Timu itafanya mawasiliano na Mkurugenzi wa Halmashauri, Katibu Tawala wa Mkoa, au Kikosi Kazi cha Upimaji cha LGDG kuhusiana na maendeleo au changamoto zilizojitokeza wakati wa zoezi la upimaji ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa wakati kutegemea aina na ukubwa wa changamoto.

(v) Timu itafanya vikao vifupi na wakuu wa Idara kwa ajili ya kuwasilisha matokeo ya awali ili kuleta uwazi, majadiliano na kuhakiki matokeo hayo ya mwisho wa zoezi la upimaji kwa kila MSM. Muhtasari wa mkutano huo utaandaliwa na kiongozi wa Timu ya Upimaji ya Mkoa na kusainiwa na pande zote kama ushahidi wa masuala yaliyojadiliwa na kukubaliana.

(vi) Timu iandae taarifa ya kila MSM kufuatana na fomati iliyoelekezwa. Kiongozi wa Timu atawajibika kuratibu uunganishaji na uwasilishaji wa taarifa kwa njia ya kielektnoniki kwenye Kikosi Kazi cha Upimaji cha LGDG, si zaidi ya siku mbili (2) baada ya kukamilika kwa zoezi la upimaji kwenye MSM husika. Nakala za taarifa ya upimaji na mihtasari ya mikutano ya mrejesho itaambatishwa kwenye taarifa hizo.

(vii) Kiongozi wa Timu ataandaa taarifa ya upimaji ya jumla ya mkoa ikielezea mambo yaliyojiri, matatizo na changamoto zilizopatikana kuhusiana na zoezi la upimaji kwenye mkoa husika na kuwasilisha taarifa hiyo kwa njia ya kielektroniki kwenye Kikosi Kazi cha Upimaji cha LGDG na kwa Katibu Tawala wa Mkoa ndani ya siku tatu (3) baada ya kukamilika kwa zoezi la upimaji.

(viii) Baada ya kupokea taarifa ya upimaji Kikosi Kazi cha Upimaji cha LGDG kitafanya mapitio kupata ufafanuzi kutoka kwa Timu za Upimaji za Mikoa, kufanya mabadiliko yoyote yatakayoonekana ni muhimu na kuandaa Taarifa ya Kitaifa.

(ix) Kikosi Kazi cha Upimaji cha LGDG pia kitachambua masuala yaliyojiri kwenye taarifa za upimaji kwa maboresho ya siku za usoni za mchakato wa upimaji iliyojumuishwa kama sehemu ya taarifa fupi ya kitaifa.

(x) Kikosi Kazi cha Timu ya Upimaji kitawasilisha taarifa fupi ya kitaifa pamoja na taarifa zote za upimaji za mikoa na MSM kwa katibu mkuu OR- TAMISEMI kwa hatua zaidi.

ZINGATIA: Kipengele cha (i) – (vii) vinapaswa kufanyika mwezi Agosti wakati vingine vyote vitafanyika mwezi Septemba mwaka huohuo.

Mchakato wa Uidhinishaji wa Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG)

Katibu mkuu wa OR-TAMISEMI atawasilisha taarifa ya kitaifa kwenye kamati ya kitaalamu ya LGDG na kamati hiyo itafanya mapitio, kujadili na kutoa maoni yake kwa ajili ya kuiwasilisha kwenye kamati kuu ya kitaifa ya LGDG ili kupitiwa na kuidhinishwa.



Usambazaji wa Matokeo

MSM na Sekretarieti za Mikoa zitapatiwa nakala za kila taarifa za upimaji na ile ya kitaifa. Taarifa hizo zitajadiliwa kwenye CMT, Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango na Baraza la Madiwani ili hatua nyingine ziweze kuchukuliwa. Muhtasari wa matokeo ya upimaji itachapishwa kwenye magazeti yanayosomwa zaidi na wananchi kwa ajili ya upelekaji wa taarifa. Hali kadhalika, MSM zitatakiwa kusambaza muhtasari wa matokeo ya upimaji kwa kuyabandika kwenye mbao za matangazo kwenye ngazi za juu na ngazi za msingi.

Rufaa na Hatua za Marekebisho

Rufaa

Halmashauri zimepewa fursa ya kukata rufaa kuhusu matokeo ya upimaji ndani ya muda uliowekwa. Pale ambapo MSM haijaridhika na matokeo ya upimaji kwa sababu ya kuondolewa kwa baadhi ya maeneo au kwa sababu ya taarifa kuwa na makosa basi MSM itandaa nia ya kukata rufaa kwa katibu Mkuu OR- TAMISEMI ambako baadae MSM itawasilisha malalamiko yake rasmi kwa maandishi, nakala kwa Katibu Tawala wa Mkoa ndani ya siku saba (7) baada ya kupokea taarifa ya upimaji. Rufaa hiyo lazima iambatane na ushahidi utakaosaidia rufaa hiyo ikiwemo mihtasari ya mikutano baina ya CMT na Timu ya Upimaji. Katibu Mkuu OR- TAMISEMI ataijibu rufaa ndani ya siku saba (7) baada ya kuipokea rufaa hiyo. Iwapo MSM haitaridhika na majibu ya Katibu Mkuu inaweza kukata rufaa yake kwa kuiandikia Kamati Kuu ya Kitaifa ya LGDG kupitia OR- TAMISEMI ndani ya siku 14 baada ya kupokea maamuzi ya rufaa ya awali kutoka kwa KM – OR TAMISEMI

Hatua za Marekebisho

- MSM zitakazoshindwa kukidhi vigezo vya msingi zitaandaa mpango kazi utakaoainisha kasoro na hatua za marekebisho ndani ya miezi sita kwa mwaka huo huo wa fedha. Mpango kazi huo utakuwa ndiyo makubaliano baina ya MSM na OR- TAMISEMI na utasainiwa na MSM, Sekretarieti za Mikoa na OR- TAMISEMI.

- MSM itatoa taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mpango kazi kwa kila robo mwaka kwenye OR – TAMISEMI kupitia Sekretarieti ya Mkoa. Sekretarieti ya LGDG na Sekretarieti ya Mkoa ambamo MSM zipo zitasimamia kwa karibu utekelezaji wa mpango kazi.